BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA KUMI NA TANO</u>

<u>Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 10 Juni, 2024</u>
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. <u>HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:</u>

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2024/2025.

<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:</u>

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Mwaka 2024/2025.

## II. <u>MASWALI:</u>

<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora :</u>

133. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali imekuwa ikiwasomesha watumishi wa umma ili kuongeza ujuzi na kuweza kuzisaidia taasisi na mashirika ya Serikali katika kuongeza ufanisi na tija. Pamoja na juhudi hii ya Serikali ya kuwasomesha watumishi wake, kumekuwa na shida ya kuwabadilisha kada watumishi hao.

(b) Je, ni taratibu gani huhitajika ili mfanyakazi aweze kubadilishwa kada ya awali na kumuweka katika kada mpya aliyoisomea.

(b) Je, ni watumishi wangapi wamebadilishwa kada tokea mwaka 2020 na katika fani zipi.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kurahisisha utaratibu wa kuwabadilisha kada watumishi wake ili kuwatia motisha na kuwaongezea ujuzi wa fani wanazozitumikia.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

217. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Baada ya kazi kubwa inayofanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya barabara.

Je, ni mikakati gani Wazanzibari watarajie katika kuupendezesha mji wote wa Zanzibar ili uwe na muonekano mpya wa kisasa.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

231. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kukua kwa lugha adhimu ya Kiswahili duniani hivi sasa, kunakwenda sambamba na mahitaji makubwa ya soko la vitabu, majarida, magazeti na vipeperushi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia waandishi chipukizi kuweza kumudu kupata mikopo nafuu itakayowawezesha kuchapisha kazi zao na kuziingiza kwenye soko.

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwa na uwekezaji wa kimkakati wa kuwekeza sasa kwenye makampuni ya uchapishaji wa vitabu na majarida mbali mbali ya lugha ya Kiswahili.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

43. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Baadhi ya wananchi wanapotaka kuanzisha vyuo vya binafsi, wakati wa kuanzisha vyuo wanapoenda NACTE hushauriwa wasitumie mtaala wa Tanzania Bara na badala yake waende Wizarani Zanzibar ili watumie mtaala wao ambao haupo na hulazimika kuutumia mtaala huo ambao hulipia zaidi ya 1,500,000/=.

    Je, Wizara yako inaliangalia vipi suala hili.

201. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Baada ya uzinduzi wa vitalu vya mafuta kwa mafanikio, Je, ni lini Wizara inafikiria kuanzisha kozi za elimu ya mafuta kwenye vyuo na taasisi zetu mbali mbali nchini.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

99. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, mawasiliano na Uchukuzi:

    Tunaipongeza Serikali kwa kufikia maamuzi na kupitisha bajeti kwa ajili ya ujenzi wa barabara za ndani katika majimbo mengi ya Unguja na Pemba. Jambo hili lilileta faraja na furaha kubwa kwa wananchi wa maeneo ambayo barabara hizi zitajengwa, ikiwa ni pamoja na wananchi wa jimbo la Mtambwe ambao waliahidiwa kujengewa barabara tano (5) za ndani katika jimbo hilo.

    (a) Je, ni sababu gani zilizopelekea barabara hizo kutoendelea wakati mkandarasi alishaanza kazi ya kung'oa miti.

    (b) Je, kusimama kwa ujenzi huu hakuwezi kuleta migogoro na wakandarasi.

    (c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuwafidia wananchi ambao walipoteza vipando vyao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

87. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa huduma ya maji safi na salama ni hitaji la kila mwananchi.

Kwa nini maeneo mengi visiwani mwetu yanakosa huduma hiyo kinyume na malengo ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

232. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Ni jukumu la nani la kuwadhibiti wanyama wanaozurura ovyo mitaani.

(b) Tathmini iko vipi juu ya mahitaji ya uwepo wa madaktari wa wanyama pamoja na hospitali za dharura za kuwatibu wanyama.

(c) Ni maradhi gani sugu yanayowapata wanyama wetu yanayoshindikana kutibiwa nchini kwetu.

233. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Je, Wizara yako ina jumla ya magari mangapi yanayotumika kwa shughuli za huduma za wanyama yakiwemo ya dharura (Ambulance).

(b) Ni kwa kiasi gani wanyama wenye uhitaji wa tiba na afya waliopo vijijini wanafikiwa kwa urahisi na kwa wakati.

(c) Je, ni changamoto zipi za msingi zinaikumba Idara ya Wanyama katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Wizara ya Afya:**

143. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya

Katika kutafuta namna ya kuboresha huduma za afya, Serikali imeamua kubinafsisha baadhi ya huduma hizo kwa makampuni mbali mbali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma bora zaidi, na makampuni hayo yamekuwa na watendaji wao wanaotumika kutoa huduma husika.

(a) Je, njia gani zilitumika wakati wa zoezi zima la kuzipata kampuni hizo.

(b) Je, njia iliyotumika ni muafaka kupata watendaji waliokidhi vigezo vilivyotakiwa.

(c) Je, Serikali imeshafanya tathmini yoyote na kujiridhisha kuwa huduma zinazotolewa na watendaji wa makampuni hayo, zinawaridhisha wananchi wake.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**10 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**